

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI

Telegramu "NISHATI".
Simu: + 255-26-2322018
Nukushi: +255-26-2320148



Mji wa Serikali - Mtumba,
S. L. P 2494,
DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Mwaliko wa Kushiriki Mkutano na Maonesho ya 10 ya Petroli ya Afrika Mashariki (the 10th East African Petroleum Conference and Exhibition 2023 – EAPCE'23)

Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na taasisi zilizo chini yake (EWURA, PURA, TANESCO, TPDC, PBPA na REA) inachukua fursa hii kuwakaribisha kushiriki katika Mkutano na Maonesho ya 10 ya Petroli ya Afrika Mashariki (EAPCE'23) yatakayofanyika Jijini Kampala – Uganda kuanzia tarehe 09 hadi 11 Mei 2023.

Mgeni rasmi katika Mkutano huo anatarajiwa kuwa **Raisi wa Jamhuri ya Uganda, Mhe. Yoweri Kaguta Museveni** na utahudhuriwa na wadau zaidi ya 1,000 kutoka nchi wanachama wa Afrika Mashariki.

Lengo kuu la Mkutano huo ni kuvutia uwekezaji katika sekta ya mafuta na gesi asilia kwa kutangaza shughuli za utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia zinazoendelea ndani ya ukanda wa Afrika Mashariki pamoja na kubadilishana taarifa kuhusu hali ya maendeleo ya sekta hiyo katika kila Nchi Mwanachama ikiwemo miradi inayotekelezwa na fursa za uwekezaji zilizopo.

Kutokana na ukubwa na umuhimu wa tukio hili, Wizara ya Nishati pamoja na taasisi zilizo chini yake inawaalika wadau wote wa sekta ya nishati na Watanzania wote kwa jumla kushiriki katika Mkutano wa 10 wa Petroli wa Afrika Mashariki.

Kwa maelezo zaidi kuhusiana na Mkutano huo, tafadhali piga au tuma ujumbe mfupi wa maneno kwenda namba **0688039568, 0754896161** au **0757935727**.

EAPCE 2023, kwa maendeleo endelevu ya rasilimali za mafuta na gesi asilia katika nchi wanachama wa Afrika Mashariki.

**KATIBU MKUU
WIZARA YA NISHATI**